

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**KIKAO CHA NANE**

**05 SEPTEMBER, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 05 SEPTEMBER, 2024**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**126. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Kituo cha Afya Arash.

**127. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Magadu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

**128. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Watoto Wenye Mahitaji Maalum katika Mkoa wa Simiyu.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**129. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini posho ya kujikimu isilipwe sawa kwa Wafanyakazi wanaojitolea ili kuondoa matabaka ya malipo kulingana na sehemu wanazofanya kazi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**130. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, upi mkakati wa Serikali wa kukabiliana na matumizi ya mkaa na kuni nchini ili kulinda Mazingira.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**131. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Mahakama Kata ya Chikundi - Ndanda itatekelezwa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:-**

**132. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Mnada wa Mifugo uliojengwa kwa gharama ya Shilingi Milioni 600 katika Kata ya Kileo Wilayani Mwanga utafunguliwa na kuanza kazi.

**133. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itanunua Meli 8 za Uvuvi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020 - 2025.

**WIZARA YA MAJI:**

**134. MHESHIMIWA JOSEPHINE TABITHA CHAGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Mkoa wa Geita.

**WIZARA YA KILIMO:**

**135. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-



Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto zilizojitokeza kwenye mfumo mpya wa Stakabadhi ghalani wa kuuza mazao ya Dengu na Mbaazi.

**III. UCHAGUZI WA MBUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI (EALA):**

**DODOMA  
05 SEPTEMBER, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

